JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS NA TAWALA ZA MIKOA (OR – TAMISEMI)
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO

SHULE YA SEKONDARI MKULAZI,
S.L.P 1927,
MOROGORO.
TAREHE .....

KUMB. Na: MKSS/S.4613/JI/VOL.1/09

Mwanafunzi: .....
S.L.P.....
MOROGORO.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MKULAZI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO MWAKA 2021

1.0 Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (1) 2021 katika shule hii. Mwisho wa kuripoti kidato cha kwanza Tarehe ..... Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa atakayechelewa kuripoti. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza Tarehe ..... .

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

2:1 SARE ZA SHULE

a) Sare ya shule hii ni rangi ya kijani kwa suruali kwa wavulana na sketi kwa wasichana.
b) Mashati meupe kwa wavulana na wasichana,
c) T-shirt ni rangi ya njano wavulana na wasichana,
d) Hijab ni rangi nyeupe kwa wasichana,
e) Sare za michezo Track suit ya rangi bluu bahari na raba nyeupe au viatu vya michezo kwa wavulana na wasichana,
f) Viatu vyeusi vya kamba vyenye visigino vifupi, soksi nyeusi ndefu kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana,
g) Mkanda rangi nyeusi kwa wavulana.

NB: Tafadhali zingatia rangi ya kipande cha kitambaa kilichoambatanishwa na fomu hii vinginevyo sare hiyo haitapokelewa, zingatia mishono ya suruali na sketi yenye maadili ya mwanafunzi.

2:2 TAALUMA

a) Kila mwanafunzi aje na madaftari 10 makubwa (counter books),
b) Kalamu za wino blue au nyeusi na kalamu za risasi (penseli),
c) Aje na begi la kubebea madaftari yake na vifaa vingine,
d) Kila mwanafunzi aje na mkebe (mathematical set), rula na kamusi (dictionary) ya English to English,
e) **Aje na meza 1 pamoja na kiti 1**.(Asipoleta meza na kiti hatapata meza na kiti za kutumia yeye)

2:3 VIFAA VYA USAFI NA KILIMO

i) Mifagio ya ndani na nje (1),
ii) Jembe (1),

iii) Ndoo ndogo lita 10 (1),
iv) Kwanja/fyekeo (1),
v) Panga (1),
vi) Reki (1).

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu na. 25 ya mwaka 1978 aidha inazingitia miongozo yote inayotalewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu,
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation),
d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa,
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wake katika shule hii,
f) Kutunza usafi wa mwili na Mazingira ya shule,
g) Kuvaa sare ya shale wakati wote anapotakiwa uwapo shuleni na utakapotakiwa,
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI AKAFUKUZWA SHULE

1. Wizi,
2. Uasherati na ushoga,
3. Ubakaji,
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.,
5. Kupigana na kupiga,
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma,
7. Kudharau Bendera ya Taifa,
8. Kuoa au kuolewa,
9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule,
10. Kutoa mimba,
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu,
12. Kukataa adhabu kwa makusudi,
13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU

Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospital ya serikali. Fornu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

NB: Tatadhali soma kwa umakini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII

.....

MARY RICHARD (0754 475 755)
MKUU WA SHULE

THE HEADMISTRESS
MKULAZI SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 1927
MOROGORO

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical officer in respect of form one entrant.

PUPIL'S FULL NAME.....

AGE..... (YEARS).....

BLOOD COUNT (RED AND WHITE).....

STOOL EXAMINATION.....

URINE ANALYSIS.....

SYPHILLIS TEST.....

T.B. TEST.....

EARS.....

CHEST.....

ABDOMEN.....

SPLEEN.....

PREGNANCY.....

ADDITIONAL INFORMATION

E.g. Physical defects or impairments, infection chronic of family diseases Etc

.....

.....

.....

.....

.....

.....

I certify that above is fit/unfit for admission into a day/boarding school

Signature:.....Designation.....

Station: .....

Date .....

Note: Medical officer, at the time of examination please treat the individual for any illness

You note/employee: This complete form should be sent to the Head of the school.

No pupil or person may be enrolled without certification of physical fitness.